



Tom muuza ndizi

 Humphreys Odunga

 Zablou Alex Nguku

 Matteo E. Mwita

 2

 Kiswahili SW



Tom anabeba tenga la ndizi zilizoiva.



Tom anaenda sokoni kuuza ndizi.



Sokoni watu wananunua matunda.



Lakini hakuna anayenunua ndizi za Tom.
Wanapenda kununua matunda kutoka kwa
akina mama.



“Kwenye jamii yetu, ni wanawake pekee ndio wanaouza matunda,” watu wanasema. “Ni mwanamume wa aina gani huyu?” watu wanahoji.



Lakini Tom hakati tamaa. Anaita, “Nunua ndizi zangu! Nunueni ndizi zangu tamu zilizoiva!”



Mwanamke mmoja anachukua kichane cha ndizi kutoka kwenye tenga. Anaziangalia ndizi kwa umakini.



Mwanamke ananunua ndizi.



Watu wengine wanakuja kwenye kichanja.
Wananunua ndizi za Tom na kuzila.



Mara, tenga linakuwa tupu. Tom anahesabu pesa alizopata.



Tom ananunua sabuni, sukari, na mkate.
Anaweka vitu kwenye tenga lake.




Tom anajitwisha tenga kichwani na kwenda nyumbani.




Global Storybooks

globalstorybooks.net

Tom muuza ndizi

 Humphreys Odunga

 Zablon Alex Nguku

 Matteo E. Mwita

